UPENDO WA MILELE WA MUNGU

“Bwana alinitokea zamani, akisema, naam nimekupenda kwa upendo wa milele: ndiyo maana nimekuvuta kwa fadhili zangu,” Yeremia 31:3. Zingatia kipande kinachosema, “nimekupenda kwa upendo wa milele” Kipande hiki kitakuwa ndiyo maada yangu katika makala mbili tatu zijazo.

Twasoma habari ya upendo wa ajabu wa Mungu ulio wa milele. Upendo ambao ulikuwa na nguvu ya kutosha kumfanya amtume mwanawe kwa ajili ya dhambi zetu Yohana 3:16; Warumi 5:8. Kwa hivyo tunayajua matokeo ya pendo lake. Kwa miaka mingi alifanya kazi kubwa ya kumleta mwanawe panapo utimilifu wa wakati Wagalatia 4:4. Aliacha mwanawe afe kwa ajili yetu tulipokuwa hatustahili chochote zaidi ya ghadhabu ya Mungu, Warumi 3:10; 3:33. Ingawaje tunajua matokeo ya upendo wake huu wa ajabu, naya kuwa Paulo anatufundisha kuutuambua na kuujua upendo wa Kristo Waefeso 3:17-18. Kwa kusemwa yote haya, hivi tunaitambua kweli siri ya upendo wake wa ajabu?

Ni dhahiri kwamba pendo lake kwetu ni la ajabu! Huku tumejaa kutu ya dhambi na kuvunjika kwa namna mbalambali, Bado Mungu alitupenda, akamtuma mwanawe ili atupe uzima, Warumi 5:8. Mungu alipomwongea uzima Hezekia, Hezekia alisema “…Lakini kwa kunipenda umeniokoa na shimo la uharibifu”,” Hezekiah 38:17. Na ashukuriwe Mungu kwa kutupa njia ya kutuokoa leo kutoka kwenye mioto ya Jehanamu.

Pendo lake ni Siri! Ni jinsi gani aliye mtakata kabisa, mwenye haki na mtakatifu akampenda mwenye dhambi kafiri? Habakuki aliandika katika 1:13, “Wewe uliye na macho safi hata usiweze kuangalia uovu, wewe usiyeweza kutazama ukaidi,” Hata hivyo kutokana na neema na huruma yake (Waefeso 4:1-14) alitutazama viumbe wake tulioanguka na akatuongezea tunu ya mwanawe. Ni dhahiri Pendo lake lapita fahamu zetu kuelewa kwa uwezo wetu wenye ukomo. Lakini haimaanishi kuwa hatuwezi kuelewa kuwa pendo lake ni “la ajabu kupita fahamu zetu.” Mtunga zaburi alisema “Neno hili limetoka kwa BWANA, nalo ni la ajabu machoni petu” Zaburi 118:23

Anatupenda kwa sababu ni Baba yetu, Mathayo 6:1. Wengi wetu tulibahatika kuwa na baba zetu wanaotupenda. Nasi tuliokuwa na baba wenye upendo, tulikuwa na baba ambao upendo wao ni sehemu ya upendo utokao kwa Baba aliye juu. Tuliposononeka, baba zetu wa duniani walitaka kutufurahisha. Tulipoumizwa walitaka kutuondolea maumivu. Hata kama ulimuudhi baba yako, unajua ya kuwa bado anakupenda. Hata kama ulikosa, au ulivunja chombo fulani, ulijua kuwa atatengeneza! Ndivyo ilivyo kwa Baba yetu wa mbinguni na kisha kwa wengine. Katika Zaburi ya 103:13-17, Daudi alisema “Kama vile baba awahurumiavyo watoto wake, Ndivyo BWANA awahurumiavyo wamchao. Kwa maana Yeye anatujua umbo letu, na kukumbuka ya kuwa sisi tu mavumbi. Mwanadamu siku zake ni kama majani, kama ua la kondeni ndivyo asitawivyo. Maana upepo hupita juu yake, kumbe haliko! Na mahali pake hapatalijua tena. Bali fadhili za BWANA zina wamchao, tangu milele hata milele, na haki yake ina wana wa wana.”

Upendo Wa Milele Wa Mungu - #2

“Bwana alinitokea zamani, akisema, naam nimekupenda kwa upendo wa milele: ndiyo maana nimekuvuta kwa fadhili zangu,” Yeremia 31:3. Zingatia kipande kinachosema, “nimekupenda kwa upendo wa milele”

Upendo wa milele wa Mungu unashuhudiwa katika huruma yake juu yetu, Waefeso 2:1-4. Kwa kule kuwa wachanga na wapweke katika anga za shetani, tumejikuta sote tumemwacha akatupumbaza na kutupeleka shimo lenye lindi la tope. Kama hayawani mbaya “Nachelea; kama yule nyoka alivyomdanganya Hawa kwa hila yake; asije akawaharibu fikra zenu, mkauacha unyoofu na usafi wa Kristo,” 2 Wakorintho 11:3. Ingawaje tumeharibika, Upendo wake bado umenyooshwa kutoka mbinguni juu ili kunyakua kutoka shimo la dhambi.

Pili, Mungu anatupenda kama ukweli unavyoshuhudu, “Mikono yako ikanifanya, ikanitengeza,” Zaburi 119:733. Tu kazi ya mikono yake, tumeumbwa kwa mfano wake, Mwanzo 1:26. Anaupenda uumbaji wake kwa sababu tu mali yake. Alitufanya, alitutengeneza, na ile sura tuliyopewa itamrudia Yeye hivi punde, Muhubiri 12:1.

Tatu, Mungu wetu anatupenda kwa sababu ya nafasi ya uwezekano aliyonayo kila mmoja wetu. Bila kujali tumeangukia mbali kiasi gani, bila kujali tunawaza au kufanya mabaya kwa kiwango gani, kama tunayo pumzi bado Mungu anaona uwezekano ndani yetu. Katika Muhubiri 7:29, mwenye hekima alinena “Mungu amemfanya mwanadamu mnyofu, lakini wamebuni mavumbuzi mengi”. Kwa dakika moja mfikirie Sauli aliyeitwa Paulo. Hapakuwa na mkristo hata mmoja juu ya nchi aliyeona jema lolote kwake. Kulikuwa na dua zaidi ya moja zilizoinuliwa juu mbinguni wakristo wakimwomba Mungu awaepushe na Sauli na kundi lake la watesi. Ingawaje alipotoshwa, Mungu alikiona kitu ndani yake, akamnusuru na kumsafisha dhambi ili awe mtenda kazi wa Bwana asiyechoka, Matendo ya Mitume 22:13-16. Ndivyo ilivyo kwako. Haijalishi familia na majirani zako wanakuonaje. Wanaweza kukuona kama “kondoo mweusi” Mchafu wa hali ya juu duniani. Sawa, Mungu naye anaziona dhambi zako, lakini anaona uwezekano ulio ndani yako pia.

Upendo Wa Milele Wa Mungu – Sehemu Ya Tatu

“Bwana alinitokea zamani, akisema, naam nimekupenda kwa upendo wa milele: ndiyo maana nimekuvuta kwa fadhili zangu,” Yeremia 31:3. Zingatia kipande kinachosema, “nimekupenda kwa upendo wa milele

Upendo wa Mungu ni mkuu kama unavyoshuhudiwa katika hamu yake na dhamira ya kwamba sisi tuishi naye milele, Mwanzo 2:9. Lakini dhambi ikaingilia na kuusambaratisha mpango, Mwanzo 3:8. Mungu hakuutupilia mbali uumbaji wake. Kuanzia katika Mwanzo 3:15, alitabiri ufumbuzi kwamba ungekuja kwa njia ya “uzao wa mwanamke” ambao ungetuwezesha kuwa na makazi ya milele pamoja naye mbinguni Waebrania 11:6; Mathayo 25:46.

Pili, Upendo wa Mungu umeshuhudiwa kwa njia ya tunu ya thamani ya mwanawe pekee. Aliyetumwa ili kutukomboa, kutunusuru na kuwasafisha wale walio watiifu kwake, Yohana 3:16-21. Dhabihu hii pekee inaonyesha kina cha upendo wa Mungu kwa ajili yetu, “Bali Mungu

aonyesha pendo lake Yeye mwnyewe kwetu sisi, Kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi.” Warumi 5:8

Tatu, Upendo wa Mungu hauna mpaka kama unavyoshuhudiwa kwa uwezo wake wa kuwafikia walio mbali ili wamjie kwa njia yetu tunapobeba injili kwenda katika pande nne za nchi ili kuokoa nafsi za wanadamu wote, Mathayo 28:18. Ni shauku yake kwamba hakuna wa kupotea, bali wote wafikilie toba (2 Petro 3:9)

Nne, Upendo wa Mungu hauna mwisho. Tunaishi katika ulimwengu unaopita na vitu vyake. Tuna vikombe ambavyo ni vya kutupa, sahani, uma, tishu na mengineyo mengi. Hata vifaa vyetu vya umeme siku hizi vimetengenezwa vya kutumika na kutupwa, kwa maana kwamba ni rahisi kununua kifaa kipya kuliko kukikarabati kikiharibika. Kwa upande wa Mungu, upendo wake hauna mwisho. Hakuna tarehe ya mwisho wa matumizi. Jambo hili, Daudi alilielezea katika Zaburi ya 86:15-16 “Lakini wewe, Bwana, U Mungu wa rehema na neema, mvumilivu, mwingi na wa neema kweli. Unielekee na kunifadhili mimi:” Hakuna shaka kwamba upendo wake kwetu ni wa milele, Yeremia 31:3.

Kama watu wa Mungu na tufurahi katika pendo lake. “Kwa maana pendo la Mungu limemimininwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi.” Na kamwe usisahau kusoma, kuamini na kufurahi ndani yake. Na kujifunza Biblia, ambayo ni hazina ya pendo la Mungu